



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

**UTIAJI SAINI WA MAADILI YA UCHAGUZI WA RAIS,
WABUNGE NA MADIWANI YA MWAKA 2020**

Dar es salaam 27 Mei, 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Serikali na Vyama vya Siasa kwa pamoja leo wamejadili na kusaini maadili ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020 ikiwa ni maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Kwenye hotuba yake ya ufunguzi wa hafla hiyo yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam leo tarehe 27 Mei 2020, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji Rufaa (mst) Semistocles Kaijage amesema Tume kwa kushirikiana na vyama vya siasa na Serikali huandaa Maadili ya Uchaguzi kwa shabaha ya kuwa na uchaguzi ulio huru, wa haki, wa wazi na wa kuaminika.

Maadili hayo yatasaidia kuwa na uwanja sawa wa ushindani katika Uchaguzi na huandaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo.

Jaji Kaijage amesema kwamba mara ya mwisho Maadili yaliandaliwa na kutiwa saini mwaka 2015 na kutumika katika Uchaguzi Mkuu na chaguzi ndogo zilizofuata. Hivyo, ni muda mwafaka tena kwa vyama vya siasa, Tume na Serikali kama wadau wa Uchaguzi kuandaa Maadili kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka, 2020.

Kabla ya majadiliano hayo ya leo Tume ilishawapa Vyama vya Siasa na Serikali rasimu ya Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka, 2020 ambapo walipata fursa ya kupitia na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali.

“Tume ilipokea maoni na mapendekezo yenu ambayo yamezingatiwa katika Rasimu hii ya Maadili. Hatua hiyo ililenga kutoa mazingira bora ya kurahisisha

na kufupisha mjadala wa kikao cha leo ambacho kitahusisha Rasimu ya pili ya Maadili ya Uchaguzi,” amesema Jaji Kaijage.

Aliwakumbusha kwamba maadili haya ni maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka, 2020 na kwamba kila mhusika wa Maadili atapaswa kuyafuata kwa lengo la kudumisha amani ya Nchi na kuwa na uchaguzi ulio huru na wa haki.

“Tume imejizatiti na imejipanga kuhakikisha kuwa inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba, Sheria, Kanuni pamoja na kuzingatia masharti ya kanuni za Maadili ya Uchaguzi. Hivyo, ni matumaini yangu kuwa Serikali, viongozi wa vyama vya siasa na wagombea wa nafasi mbalimbali mtaheshimu na kuyatekeleza Maadili haya na mtawaelimisha, kuwahamasisha na kuwasisitiza wanachama wenu kuyaheshimu Maadili haya na kufuata Sheria za Uchaguzi, sheria nyingine za Nchi, kanuni, maelekezo ya Tume na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria,” amesema.

Wadau wakuu wa Maadili ni vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu, Wagombea waliopendekezwa na vyama, Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Imetolewa na;

Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga Kura